

# Jinsi ya Kufanya Kipimo cha Kujipima cha Kupima Antijeni za COVID-19 cha BinaxNOW

## HATUA YA 1

Chukua kipimo katika eneo la upimaji.

## HATUA YA 2

Kagua maelekezo yote yanayohusiana na kipimo.

## HATUA YA 3

Jipime nje ya eneo la huduma na usubiri kwa dakika 15 hadi 30 kupata matokeo yako.

## HATUA YA 4

Ripoti matokeo katika [healthvermont.gov/reportresults](http://healthvermont.gov/reportresults) na ujaze fomu fupi.

Ni muhimu kuripoti matokeo ya kipimo chako. Jibu lako ni siri.



### Huduma za Kutafsiri Lughha

1. Piga Simu 1-413-216-4975
2. Weka nambari ya PIN 6187848 na alama ya reli ("#") unapoombwa
3. Sikiliza kidokezo cha kiotomatiki na chagua lugha



**Kwa maulizo ya jumla,** msaada unapatikana kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni kwa kuwasiliana na (877) 380-3029 au [support@cic-health.com](mailto:support@cic-health.com)

# Maswali Yanayouлизwa Sana

## Je, Kipimo cha Kujipima cha Kupima Antijeni za COVID-19 cha BinaxNOW™ ni nini?

Kipimo cha Kujipima cha Kupima Antijeni za COVID-19 cha BinaxNOW ni kipimo cha biokemia cha haraka kinachokusudiwa kutambua antijeni ya protini ya nukleokapsidi kutokana na SARS-CoV-2 kutoka kwa watu walio na au wasio na dalili au sababu zingine za magonjwa ya mlipuko ili kushuku maambukizi ya COVID-19 wanapopimwa mara mbili katika siku tatu na angalau saa 36 baina ya vipimo. Kipimo hiki kimeidhinishwa kwa matumizi ya nyumbani yasiyo na maelekezo ya daktari kwa kutumia sampuli unazokusanya mwenyewe moja kwa moja kutoka kwenye usufi wa pua (matundu ya pua) kwa watu walio na umri wa miaka 15 au zaidi, au sampuli za usufi wa pua zinazokusanywa na mtu mzima kutoka kwa watoto walio na umri wa miaka miwili au zaidi.

## Je, Kipimo cha Kujipima cha Kupima Antijeni za COVID-19 cha BinaxNOW kinalinganishwa vipi na kipimo cha maabara?

Vipimo vya antijeni ni mahususi sana kwa virusi, lakini havina usahihi wa juu kama ilivyo kwa vipimo vya maabara. Hii ina maana kwamba matokeo chanya huwa ni sahihi, lakini matokeo hasi hayamaanishi hakuna maambukizi.

## Kwa nini kuna vipimo viwili kwenye kifurushi?

Kulingana na BinaxNOW, kipimo kimeundwa kwa matumizi ya bila maelekezo ya daktari/kutumia mwenyewe wakati watu wanajipima mara mbili ndani ya siku tatu, na saa 36 baina ya vipimo hivi viwili. Vipimo viwili vilivyojumuishwa huwawezesha watu binafsi kutimiza matumizi yaliiyopendekezwa.

## Je, ninapaswa kufanya nini ikiwa matokeo yangu ya kipimo ni chanya?

Iwapo utathibitishwa kuwa na virusi, hakikisha kuwa umeripoti matokeo yako kupitia kiungo kilichopo upande mwininge wa kadi hii. Kwa mwongozo wa ziada, tembelea [healthvermont.gov/covid19positive](https://healthvermont.gov/covid19positive)

## Ili kupata maelezo zaidi kuhusu Kipimo cha Kujipima cha Kupima Antijeni za COVID-19 cha BinaxNOW, tembelea [bit.ly/33uB6Tv](https://bit.ly/33uB6Tv)